

“Ninaweza kufanya mambo usiyoweza. Unaweza kufanya mambo nisyoweza. Pamoja, tunaweza kufanya mambo makuu.”

Mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel Mama Theresa, kupitia kujitolea kwake bila kuchoka kwa watoto na familia, alijua nguvu ya kushirikiana. Tunataka kuendelea kuboresha afya na ustawi wa wana-Vermont. - **hasa wale wenye mtoto au kijana aliye na mahitaji maalum ya kiafya.** Wafanyakazi wa CSHN watazisaidia familia zetu kama Gavana Phil Scott, Kamishna wa Afya Mark Levine, na viongozi wengine wanavyopanga kufungua upya biashara na huduma za afya za Vermont.

Vidokezo

- Tafadhali chukua muda kukamilisha hii [survey](#) na utoe uzoefu wako kuhusiana na **uratibu wa matunzo**. Tutatumia matokeo ya uchunguzi kutusaidia kuboresha mifumo yetu.
- Tazama mwaliko wa kuwa Mshirika wa Familia (mwaliko upo katika tafiti) na ujiandikishe.
- Tunafurahi pia kuzindua kipengele chetu cha **Kurunzi ya Familia**, fursa ya uzoefu wa familia kuelezewa, kuonekana, na kushirikishwa. Tazama familia ya Jakubiak katika ukurasa wa 2!

Rasilimali

Vermont Family Network: Washirika wetu wa Vermont Family Network wanakuletea [virtual chats](#) kwa familia. Jiunge nasi, sikiliza, ongea, na ufahamu kuwa huko peke yako.

Usambazaji wa Chakula kwa Wahitaji: Chakula kitasambazwa kwa wahitaji katika mwezi wote wa Mei. Chakula kitajumuisha mifuko/visanduku vya chakula cha FEMA, pamoja na mazao, kuku, na bidhaa zinazotokana na maziwa. Bonyeza [here](#) kwa ratiba ya usambazaji.

Family Voices: Taarifa kuhusu haki za raia, ubaguzi kwa walemavu, na huduma za kifamilia zote zinaweza kupatikana kwenye Family Voices [website](#).

Wasiliana Nasi

Wafanyakazi huko [CSHN](#) wamejitolea kukujulisha juu ya rasilimali na taarifa kwa huduma ambazo zinaweza kuihusu familia yako. Ingawa ziara za kuwaona watu ana kwa ana haziendelei kwa sasa, unaweza kutupigia simu au barua pepe wakati wowote. Tembelea tovuti yetu ili kupata [CSHN Care Coordinator](#) au tupigie kupitia 802-863-7338.

Pata habari juu ya taarifa zetu zote kwenye www.healthvermont.gov/family/special-health-needs.

Kurunzi ya Familia |

Familia ya Jakubiak



Jina langu ni Irene Jakubiak, na mume wangu Chris na mimi tuna mtoto wa miaka 13 anayeitwa Reilly ambaye ana ugonjwa aghalabu wa kubadilika vinasaba. Mabadiliko haya yanajulikana kama *KCTD7*, na Reilly ni moja ya visa nane nchini Marekani. Kuna visa visivyozidi 30 duniani kote.

Kwenye wakati huu usio wa kawaida wa janga la Covid 19, tumetoka kuwa nyumba ambayo kila mara ilikuwa na watu wanaingia na kutoka hadi kuwa nyumba ya zoom / teknolojia.

Kabla ya Covid, tulikuwa na muuguzi au mlezi wa Reilly aliyekuja siku 5-6 kwa wiki. Reilly alipata tiba ya utambuzi, kuongea na ya viungo mara mbili kwa wiki na alikuwa na shule siku tano kwa wiki. Reilly amekuwa akipewa huduma kwa kufuatwa

nyumbani kwa miaka sita iliyopita.

Tumepitia kutoka mimi kwenda nje na kufanya safari zangu hadi kuagiza kila kitu mtandaoni, ikiwa ni pamoja na vyakula! Kila wikendi tunaenda safari fupi ya (bila mwelekeo maalum!) ili Reilly na mimi tuweze kutoka nje ya nyumba. Ninajaribu kushiriki vikundi vya wazazi kupitia zoom, lakini imekuwa ngumu kutoka kuwa mtu wa kuonana na jamii hadi kuwa mtu aliyetengwa sana. Chris ameendelea kufanya kazi Green Mountain Power. Kama unavyofikiria, familia yetu imejizatiti kuhakikisha usalama wa Reilly wakati Chris anaporudi nyumbani.

Kitu kigumu zaidi kwangu ni kutojua hili litaisha lini. Ikiwa tunapata dhoruba kali ya theluji sote tunajua ni lini itaisha lakini kwa hlii nahisi kama hakuna mwisho wake.

Itawekwa katika *Kurunzi ya Familia*

tafadhali wasiliana na
charlotte.safran@partner.vermont.gov

